# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO -MASWALA YA JAMII

**Kipindi cha pili: "Ndoto Yangu"**

**Muandishi: Chrispin Mwakideu**
**Mhariri: Andrea Schmidt**

**Wahusika: Beti(12),Mwalimu (35),Darasa la mchanganyiko(12+),Eveline(19),Mapito(40),Roni(14), mkufunzi(35), Samu(14)**

## Utangulizi

Hujambo msikiliza na karibu tena katika kipindi chetu cha pili cha Noa Bongo Jenga maisha yako kuhusu maswala ya jamii – jinsi ya kuwa mshirika katika siasa. Katika kipindi kilichopita tulimuona Roni akikaribia kuwa nahodha wa timu yake ya kandanda na dadake Beti akaruhusiwa na babake kuanzisha kikundi cha kwaya katika darasa lake. Kipindi cha leo kinaanzia darasani mwa Betty katika kisa kwa jina " Ndoto Yangu."

## Sehemu ya kwanza; darasani mwa Beti

## SFX: KENGELE INALIA

1. **BETI**: Nisikilizeni wenzangu. Nanuia kuanzisha kikundi cha waimbaji ili tuweze kushindana katika tamasha la muziki. Itakuwa furaha isiyo na kifani na iwapo tutashinda basi tutapata fursa ya kumtumbuiza raisi wetu! Hata itakuwa sifa kwa shule yetu….na si mnaelewa kuenda katika ikulu ya rais ina maana tutaaaaa…..

**2.DARASA:** ( **SHANGILIO**) Tutasafiriiiiiiii! Safari ya

shuleeeee!!! Tutasafiriii!!

**SFX: DARASA LINACHACHAWA MARA GHAFLA UKIMYA UNAPATIKANA**

**3.MWALIMU:** Eeeh kimya! Kimya!....Kwanini darasa langu mumeligeuza ghafla kuwa soko? Ni nani aliyeleta kelele hizi? Kiranja wa darasa hebu nieleze!

**4.BINTI:** Mwalimu bila kukuficha ni Beti… Beti Mapito.

**5.MWALIMU**: Eti nani? Beti? Haiwezekani! Beti, umefanya nini?

**6.BETI:**( **KWA WOGA**) Samahani mwalimu. Niliwaeleza tu kuhusu tamasha la muziki na kwamba nilitaka kuanzisha kikundi cha kwaya. Basi nao wakaanza kupiga kelele.

**7.MWALIMU:** Alaa! Nafahamu. Kwa hivyo una taka kuanzisha kwaya? Wewe Betty Mapito, msichana mwenye haya zaidi darasani? Inafurahisha kweli! Sasa….. kwa kuwa unataka kuwa kiongozi…. hebu tukujaribu. Je munataka kumsikiliza Beti akiimba?

**8.DARASA**: Ndiyooo..( **KELELE**) Beti! Beti! Beti!

**9.BETI:** (**ASHIKWA NA HAYA**) Lakini mwalimu…. Sikuwa nimejitayarisha kuimba….

**10.MWALIMU:** Eti nini? Kwani umeisahau sauti yako nyumbani? Beti, kama huna ujasiri wa kusimama mbele ya darasa lako, utaweza vipi mbele ya umati mkubwa wa watu?

**11.BETI**: Sawa,( **ANASAFISHA KOO NA KUIMBA NYIMBO DUNI YA CHEKECHEA,KWA MFANO ZA NASARI)**

**12.DARASA**: Hapana…….( **KICHEKO DARASANI**)
**13.BETI**: Hiyo ilikuwa ni safisha koo tu, sasa nitawaimbia kama niko mashindanoni… Mheshimiwa mwalimu, wanafunzi wenzangu. Jina langu naitwa Bety Maputo na niko tayari kuwaimbia wimbo ninaoupenda sana.

**(BETI AIMBA WIMBO WA " MALAIKA" NA ANAUNGWA NA WENZAKE DARASANI)**

**14.DARASA**: ( **WANAPIGA VIFIJO NA NDEREMO**)

**15.MWALIMU**: Pongezi za dhati Beti.. sikujua kuwa una sauti nyororo ya kumtoa nyoka pangoni! Wanafunzi, ni nani anayetaka kujiunga na kikundi cha Beti?

**16.DARASA**: ( **WOTE**) Mimi!!!!! Mimi!! Mimi!!!

**17.MWALIMU**: Haya Beti ushapata waimbaji sasa waongoze vyema. Inapaswa ujue haitokuwa rahisi kuanzisha kitu. Kila kitu chahitaji juhudi. Haya tuendelee na masomo. Nani hayuko leo?

**18.MSIMULIZI:** Ni kweli yale mwalimu aliyoyazungumza. Tunapoteza nafasi nyingi za mafanikio kwa kuogopa kujaribu. Sasa tujiunge na Roni anapotazamia kuteuliwa kuwa nahodha wa kikosi chake cha mpira wa miguu na Eveline anapomweleza babake ndoto yake…

**<u>Onyesho la pili:Roni akiwa uwanjani</u>**

**1.KIJANA**: Roni…hapa.. nipigie pasi Roni…weka weka!!

**SFX: MPIRA UNAPIGWA**

**2.WAVULANA:** Gooooooooooal!! Baoooo!!!!!

**SFX: MKUFUNZI ANAPIGA KIPENGA**

**3.MKUFUNZI**: (**AKIPIGA MAKOFI**) Hilo ni mojwapo ya mbao mazuri niliyowahi kuyaona! Bila shaka kwenye mazoezi tu! Tukiendelea kucheza namna hii hata Brazil hawatatuweza…

**4.WAVULANA**: ( **NUN'GUNO ZA VIJANA)** Aaah acha weee kocha!

**5.MKUFUNZI:** Kama mjuavyo, zimesalia wiki chache tu kabla fainali .. kwa hivyo leo nataka kumteua nahodha wa timu. Atashikilia uongozi wa kikosi hiki iwapo sipo na mtakapokuwa kiwanjani wakati wa mchuano wa fainali..Nahodha wetu atakuwa…….

**6.WAVULANA: ( WAMSHANGILIA RONI)** Roni! Roni!

**7.MKUFUNZI**: Tulieni….tulieni…msiwe na pupa….Nahodha ni Samu.

**8.WAVULANA**: ( **WANADUWAA NA KUTOAMINI**) Haaaaa! Eti Samu?? Haaaa!

**9.MSIMULIZI:** Aha! Ama kweli hata mimi pia nimepigwa na butaa kama nyinyi. Lakini kijana wetu Roni ndiye aliyeshangazwa zaidi kwanini mkufunzi hakumchagua kuwa nahodha. Roni anaondoka kimya kimya bila kusema lolote! Zii kama maji mtungini! Wakati huo huo, Eveline ana habari kem kem kwa babake…

**<u>Onyesho la tatu: katika kituo cha polisi</u>**

**SFX: KELELE NA FIRIMBI KUTOKA KWA WASHUKIWA/ MAHABUSU**

**1.EVELINE:** Shikamoo baba…
**2.MAPITO**: Nilijuwa kuna mrembo anakuja niliposikia mahabusu wakipiga mbinja na kushangilia. Sikujua ni wewe…haya niambie kuna shida yoyote nyumbani?

**3.EVELINE:** La hasha baba..kila kitu ni salama. Niilitaka tu kuzungumza nawe faraghani kwa sababu ni muhimu. Je, una muda?

**4.MAPITO**: Eve, saa yeyote ile. Unajua wakati wowote ule niko na muda wa kuzungumza nawe……

**5.EVELINE**: Baba, tangu nilipokuwa mdogo wewe na mama mulinifunza adabu, kuwaheshimu wengine na muhimu ya yote nijitahidi kuyatimiza malengo yangu…Najuwa ninayokaribia kukueleza yatakushangaza…

**6.MAPITO: ( AKIMKATA KAULI EVELINE)** Oohh! Tafadhali, usinieleze kuwa u mja mzito.

**7.EVELINE**: Hapana baba sina mimba.. ningependa kukujulisha kwamba nataka kuwa mwanasiasa….

**8.MAPITO**: ( **ASHANGAA**) Eti una taka nini? Eti unasema unataka kuwa mwanasiasa? Eve mwanangu, je unafahamu kile unachokizungumzia?

**9.EVELINE**: Baba naomba unielewe.. nimetafakari kwa muda sasa..na hivyo ndivyo ninavyotaka.. najua bado niko mdogo lakini hiyo ni faida kwangu kwani nitapata wasaa wa kujifunza na kukomaa katika siasa kadri ninavyokua… napende kuitumikia jamii yangu na wakaazi wa hapa na bila shaka nitaweza kufanya hivyo nikiwa diwani wa Milimani…

**10.MAPITO**: ( **APUMUA PUMZI NZITO**) Aaaah! Kwanza

kijana wangu ameniambia anataka kuwa Maradona na aiongoze timu ya mpira wa miguu ya taifa hili katika kombe la dunia..Kisha malkia wangu mdogo anataka kumuiga Mariam Makeba, lakini afadhali sauti ya uimbaji anayo na anaweza kujaribu…. Na sasa wewe Eveline una umri wa miaka kumi na tisa tu na unataka kuingia ulimwengu wa siasa? Malezi yaangu ni kazi bure. Mmenishinda watoto nyie….

**11.EVELINE**: Baba, usivunjike moyo, malezi yako yametuwezesha kufikia tulipo… tutazame sisi sote tuna ndoto zetu… tunataka kuwacha sifa katika nchi yetu…

**12.MAPITO**: Lakini Eve, siasa sio ya wasichana wadogo… ni ngumu.. utapoteza marafiki na kujipatia maadui chungu tele.. na daima waandishi wa habari watakuwa wakikuandama.. maisha yako yatakuwa hayana tena usiri… haya ndiyo unayotaka?

**13.EVELINE**: Nafahamu hayo yote baba lakini ni heri kupitia hayo yote kisha nilete maendeleo katika jiji letu kuliko kutekwa nyara na madawa ya kulevya, maradhi na umaskini kama vijana wenzangu walivyoathirika…niko tayari kuwakomboa vijana wenzangu, na kuwawakilisha kama kiongozi kizazi kilichosahaulika.

**14.MAPITO**: Naona ulivyojiandaa hata umetayrisha hotuba he! … Sawa basi, nakupa kura yangu na nakuunga mkono.

**15.EVELINE**: Asante Baba .. Nitakuhitaji…

**16.MSIMULIZI**: Naam.. rafiki zangu, Eveline Mapito, akiwa na umri wa miaka kumi na tisa… anaingia uwanja wa siasa ambao daima unadhibitiwa na magwiji wa siasa na watu wenye uzofu wa miaka mingi… Amepata radhi ya babake, kwa hiyo yuko tayari kugombea udiwani wa Milimani ..Wakati huo huo katika kituo cha basi Roni hakuwepo kama ilivyotarajiwa…….

**Onyesho la nne: marafiki wa roni wanamsubiri Roni lakini hawamwoni**

**SFX: SAUTI ZA MAGARI/ MABASI ZASIKIKA**

**1.KIJANA:** Ajabu.. eh Roni leo hakuandamana nasi…

**2.SAMU**: Labda hakufurahia uteuzi wangu kama nahodha wa timu.

**3.KIJANA**: Samu.. Samahani nilisahau kukuita nahodha Samu.. Unadhani Roni atajitoa kikosini? Bila shaka ameghadhabika… Asipokuja kwa mazoezi kesho tutaaaaa….

**4. SAMU**: Fyata mdomo wako! Bla.. bla.. bla.. bla…Roni hivi, Roni vilekila kitu ni Roni tu… leo moja tu amekosa mazoezi basi nimetajiwa jina lake mara milioni… sikiliza, mimi ndiye nahodha…mutafanya vile ninavyowaamuru.. sawa? La sivyo mutajikuta nje ya timu! Basi letu ndilo hili linakuja….

**SFX: MILIO YA BASI LINALOKWENDA INASIKIKA NA KUFIFIA: NYIMBO FUPI**

<u>**NYUMBANI KWA MAPITO**</u>

**5.BETI:** Roni, hee leo umefika nyumbani mbele yangu. Si kawaida yako..Nina habari kem kem kwako.

**6.RONI**: (**UJEURI**) Sina haja. habari zako kaa nazo mwenyewe…na ni lipi la kushangaza kwa mimi kuja nyumbani mapema? Si hata mimi hapa ni kwetu ama?

**7.BETI**: Ah jamani Roni, una nini? Mbona leo wanisemea hivyo?

**8.RONI:** Kamuulize mkufunzi wetu…

**9.BETI**: Kwani leo hukufinga bao? Basi usihuzunike, kesho pia ni siku!!!

**10.RONI**: Hakuna cha kesho…. Nimetoka katika timu hiyo… sitaki tena kuichezea timu hiyo… aliyosema baba yalikuwa ya kweli. (**ABUBUJIKWA NA MACHOZI**)

**11.BETI**: Tulia Roni..tulia kaka…Nyamaza usilie.. hebu nieleze yaliyotokea…

**MWISHO WA KIPINDI CHA PILI**

**Msimulizi:**
Na wakati Roni anapomuhadithia Beti yaliyomsibu kiwanjani… tunakamilisha kipindi chetu cha pili. Kumbuka kujiunga nasi wakati mwingine pale Eveline atakapoanza harakati zake za kuwa mwanasiasa na Beti naye anakabiliwa na changamoto yake ya kwanza katika kwaya. Kumbuka unaweza kutoa maoni au kusikiza tena kipindi hiki katika tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe
Mueleze rafiki yako pia akisikilize. Kwaheri kwa sasa.